

19

**OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA HANANG**

SIMU NA :027-2530022

Nukushi Na:027-2530022

Barua pepe:ded@hanangdc.go.tz



**Ofisi ya Mkurugenzi
Mtendaji (W),
S.L.P. 2,
KATESH-HANANG,
MANYARA.**

30/08/2021

**TANGAZO LA KUKODISHA SHAMBA LA GAWAL NA BASSOTU.
ZABUNI NA. LGA/059/2021/2022/NC/06.
LIMEONGEZWA MUDA**

Halmashauri ya Wilaya ya Hanang inawatangazia wananchi wote, watu binafsi na Makampuni kuomba Zabuni ya ukodishaji wa mashamba ya Halmashauri yaliyopo eneo la Gawal lenye ukubwa wa ekari mia sita arobaini na tisa (649) na Bassotu lenye ukubwa wa ekari elfu tisa (9000). Mashamba yako kwenye maeneo mazuri yenye udongo wenye rutuba.

MASHARTI YA ZABUNI

1. Mwombaji wa Zabuni anatakiwa kulipa ada ya maombi ya Zabuni kiasi cha Tshs 50,000/= benki ya NMB baada ya kupewa Bill na Mhasibu wa Mapato Halmashauri ambayo haitarudishwa.
2. Mwombaji wa Zabuni atapewa nyaraka za Zabuni "Tender Document" na Katibu wa Bodi ya Zabuni siku za kazi kuanzia Jumatatu hadi Ijumaa saa 1:30 asubuhi hadi saa 9:30 alasiri kuanzia tarehe 31/08/2020 hadi tarehe 08/09/2021 Halmashauri ya Wilaya ya Hanang katika ofisi ya manunuzi namba 19.
3. Mwombaji atakayeshinda Zabuni ataingia Mkataba wa msimu moja tu baada ya kulipia ekari alizoomba, kuanzia September, 2021 hadi August, 2022 na haruhusiwi kupanda mazao ambayo ukomavu/uvunaji wake utavuka msimu mwingine.
4. Mwombaji atakayeshinda Zabuni atatakiwa kulitumia shamba hilo kwa shughuli za kilimo tu na siyo shughuli nyingine kama vile ufugaji au uchungaji wa mifugo na ikiwa atafanya shughuli ambazo sio za kilimo Halmashauri itamnyang'anya shamba hilo bila kurejeshewa au kurudishiwa fedha za ukodishaji.

5. Ikiwa Mzabuni hatawuna mazao kutokana na hali ya hewa yaani ukame, mafuriko au wadudu waharibifu na mambo mengine ambayo yanafanana na haya, Halmashauri haitahusika na hasara hiyo.
6. **Mzabuni atalazimika kutumia shamba kwa kuzalisha mazao ya kipaumbele ambayo ni Ngano na alizeti/kartamu kinyume na hapo atakuwa amekiuka maagizo ya serikali na hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yake..**
7. Halmashauri haitahusika na hasara itakayojitokeza katika kulima shamba atakalokodishiwa Mzabuni mfano:- ulinzi wa shamba, uharibifu unaotokana na mifugo na mengine yanayofanana na hayo maana yake ni kwamba majukumu yote yanahusu shamba atakalokodishiwa ni juu ya Mzabuni kuanzia Septemba 2021 hadi August 2022
8. **Mzabuni anatakiwa kutaja bei ya kukodisha shamba kwa ekari moja.**
9. Mzabuni anatakiwa kutoharibu makinga maji "Contours" ambayo yapo katika shamba kwa kuyalima au kuyaondoa.
10. Mzabuni atatakiwa kulipa fedha zote za ukodishaji wa shamba ndani ya siku kumi na nne (14) baada ya kupewa barua ya kukubaliwa na ataingia mkataba na kupimiwa ekari alizolipia na kuoneshwa eneo lake ndani ya siku saba (7) baada ya kulipia.
11. Kama kutatokea kutoeleweka au kutoelewana katika utekelezaji wa sharti lolote la Mkataba utakaofungwa kati ya Halmashauri na mshindi wa Zabuni (Mkulima) pande zote mbili zitakaa na kutatua tatizo kwa njia ya majadiliano. Ikiwa majadiliano yatashindwa kuleta muafaka suala hilo litapelekwa kwa msuluhishi ambaye ni Meneja wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) tawi la Katesh na ikiwa usuluhishi utashindikana shauri la suala hilo litapelekwa Mahakamani.
12. Mwombaji wa Zabuni anaweza kupewa idadi ya ekari alizoomba au kupewa pungufu kwa kutegemea idadi ya waombaji.
13. **Mwombaji ataje eneo la shamba aidha Gawal au Bassotu kwenye barua yake ya maombi na ekari anazotaka na bei kwa kila ekari.**

Barua zote za maombi ziandikwe kwa anuani ifuatayo:
KATIBU WA BODI YA ZABUNI
HALMASHAURI YA WILAYA YA HANANG,
S.L.P 2,
KATESH – HANANG

l
ri
o
ia
Jili
au

Juu ya bahasha iandikwe **ZABUNI YA UKODISHAJI SHAMBA LA HALMASHAURI LILILOKO GAWAL AU BASSOTU.**

14. Mwisho wa kuleta maombi na kupokea maombi ya Zabuni ni siku ya Jumatatu tarehe 08/09/2021 saa 5:00 asubuhi kwenye ukumbi wa Halmashauri ya Wilaya ya Hanang.
15. Maombi ya zabuni ambayo hayataletwa na kupokelewa na kusomwa siku ya ufunguzi hayatakuhalika.


Jenifa C. Omolo

**MKURUGENZI MTENDAJI (W)
HANANG'**

**MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA YA
HANANG**

NAKALA:

1. Ofisi ya Katibu Tawala.
S.L.P 10
KATESH/HANANG'
2. Watendaji wa Kata
3. Mbao za Matangazo

-Wilaya ya Hanang'

- Wajulisheni wakulima katika Kata zenu.